

Je, PAIN ni nini?

Jaribio la Mkakati wa Kutumia Analgesia Kabla ya Kufika Hospitalini, au kwa neno rahisi PAIN, ni utafiti unaofanywa ili kulinganisha dawa mbili za maumivu, fentanyl na ketamine, kwa wagonjwa walio na majeraha ya kiwewe ambao wanahitaji tiba ya maumivu kabla hawajaenda hospitalini.

Udhibiti wa maumivu baada ya jeraha baya ni sehemu muhimu ya kumtunza mgonjwa aliyejeruhiwa. Opioidi, kama fentanyl, hutumiwa sana kutibu maumivu. Utafiti huu unalinganisha fentanyl na ketamine, ambayo si opioidi, ili kubaini ikiwa watu wana madhara machache au mabaya kidogo kwa dawa moja dhidhi ya nyingine. Tutaangalia matokeo kutoka kwenye utafiti huu ili kuelewa vizuri njia bora ya kutibu maumivu kwa wagonjwa wa kiwewe wa siku zijazo.

Je, ni nini kinachofanya utafiti huu kuwa wa Kighairi cha Idhini ya Ufahamu (EFIC)?

Tembelea kiungo au uliza timu ya utafiti (PAINStudy@uvmhealth.org) maelezo kuhusu sababu ya utafiti huu kufanywa na kighairi cha idhini ya ufahamu ›
<https://www.litesnetwork.org/projects/emergency-research>

Je, utafiti huu unadhibitiwa vipi?

Tembelea kiungo au uliza timu ya utafiti (PAINStudy@uvmhealth.org) maelezo kuhusu utafiti huu na nyingine zote za EFIC zinavyodhibitiwa na kufuatiliwa ›
<https://www.litesnetwork.org/projects/emergency-research>

Je, ni nani atakayeshirikishwa?

PAIN itashirikisha watu wazima ambao:

- Ni wanaume wa umri wa miaka 18 na zaidi na wanawake wa umri wa miaka 50 na zaidi
- Wagonjwa waliojeruhiwa vibaya wanaohitaji dawa ya maumivu kupitia ndani ya mshipa
- Wagonjwa wanaosafirishwa kwenye hospitali inayoshiriki katika PAIN

Je, utafiti huu unafanywa wapi?

Utafiti huu unafanywa kwenye vituo vifuatavyo vya kiwewe kote nchini:

- Hospitali ya UPMC Presbyterian na Hospitali la UPMC Mercy (Pittsburgh, PA)
- Hospitali Kuu ya Allegheny (Pittsburgh, PA)
- Hospitali ya Cooper University (Camden, NJ)
- Hospitali ya Froedtert (Milwaukee, WI)
- Kituo cha Matibabu cha UC San Diego (San Diego, CA)

- Hospitali ya Kuu ya Zuckerberg San Francisco (San Francisco, CA)
- Kituo cha Matibabu cha University of Cincinnati (Cincinnati, OH)
- Hospitali ya University of Utah (Salt Lake City, UT)
- Kituo cha Matibabu cha Carolinas (Charlotte, NC)
- Hospitali ya Robert Packer (Sayre, PA)
- Kituo cha Matibabu cha University of Vermont (Burlington, VT)
- Hospitali ya University of Wisconsin University (Madison, WI)

Je, utafiti huu utadumu kwa muda gani?

Utafiti huu utawaandikisha hadi wagonjwa 994 kwa miaka kadhaa. Kama ilivyo kwa miradi yote ya LITES EFIC, habari kwenye hali ya utafiti zitachapishwa kwenye <https://clinicaltrials.gov/study/NCT05437575>

Je, ni nani anayefadhili utafiti huu?

Utafiti huu unafadhiliwa na Idara ya Ulinzi (DoD) mkataba W81XWH-16-D-0024, Agizo la Kazi W81XWH19F0539 kwa lengo la kutoa mbinu na mikakati inayotokana na ushahidi na kuokoa maisha kwa ajili ya kutoa utunzaji bora wa kiwewe.

Kwa nini udhibiti wa maumivu katika mazingira ya kabla ya kuenda hospitalini?

Wagonjwa wa kiwewe walio na majeraha mabaya wanahitaji kupata dawa za maumivu haraka. Kumpa mgonjwa dawa ya maumivu haraka iwezekanavyo baada ya jeraha baya kuna manufaa mengi, ikiwa ni pamoja na:

- Kupunguza kuteseka
- Waruhusu watoa huduma wa EMS kutoa tiba za kuokoa maisha (mfano, tourniquets, kufunga kwa kitata) kwa urahisi zaidi
- Inaweza kupunguza matatizo ya afya yanayosababishwa na jeraha
- Inaweza kupunguza matatizo ya muda mrefu kama vile maumivu sugu na maradhi ya msongo wa mawazo baada ya kiwewe (PTSD)

Kwa nini dawa hizi ni sehemu ya utafiti ikiwa zote zinatumiwa na madaktari wasaidizi?

Udhibiti wa maumivu baada ya jeraha baya ni sehemu muhimu ya kutunza mgonjwa aliyejeruhiwa. Opioidi, kama fentanyl, hutumiwa sana kutibu maumivu. Utafiti huu utalinganisha fentanyl na ketamine, ambayo si opioidi, ili kuona ikiwa watu wana madhara machache au mabaya kidogo kwa dawa moja dhidi ya nyingine. Fentanyl na ketamine zinatumiwa kwa sasa kutibu maumivu kwa wagonjwa kabla hawajaenda hospitalini, lakini haijulikani ikiwa moja ni salama kwa wagonjwa walio na majeraha ya kiwewe. Tunafanya utafiti huu ili kujua ikiwa dawa moja ni salama kuliko nyingine.

Je, hatakari za dawa hizi ni zipi? Je, kuna manufaa yoyote?

Wagonjwa walio katika utafiti watakata fentanyl au ketamine kwa ajili ya kudhibiti maumivu.

Dawa yoyote ya maumivu ina hatari zinazoweza kutokea; hata hivyo, ni nadra haswa katika dozi chache utakazopewa katika utafiti huu. Fentanyl inaweza kuhusishwa na shinikizo la chini la damu, viwango vya chini vya oksijeni na hitaji la tyubu ya kupumulia. Katika hali nyingine, ketamine inaweza kusababisha njozi, fadhaa, wasiwasi, au hisia za kujitenga.

Hatuna uhakika ikiwa kuna manufaa ya kupata dawa moja dhidi ya nyingine, lakini watafiti wanadhani kwamba dozi chache za ketamine zinaweza kuwa bora kupunguza hatari ya kifo na madhara mabaya ya afya kwa wagonjwa waliojeruhiwa vibaya ambao wana maumivu.

Je, watu wanaandikishwa katika utafiti vipi?

Watu wanaweza kuandikishwa katika utafiti wa PAIN ikiwa wana majeraha mabaya, wanahitaji dawa ya maumivu na wanapelekwa kwenye hospitali inayoshiriki katika utafiti wa PAIN.

Kwa kawaida, lazima watafiti wamwombe mtu idhini kabla hajashiriki katika utafiti – hii inamaanisha kusoma taarifa, kuzungumza na madaktari na wauguzi na kupata muda wa kufikiria kuhusu ikiwa angependa kujiunga. Lazima majeraha mabaya ya kiwewe yatibiwe mara moja, hivyo huenda kusiwe na muda wa mtu aliyejeruhiwa kutoa idhini ya jaribio la PAIN. Wakati mwingine watafiti wanaweza kuzungumza na familia ya mgonjwa ili kuomba idhini. Hata hivyo, katika hali ya dharura ya jeraha la kiwewe, familia mara nyingi haipo au haiwezi kupatikana kabla ya mtu aliyejeruhiwa kutibiwa.

Utafiti huu hauwezi kufanywa bila ruhusa maalum ya kuwashirikisha watu kabla ya kupata idhini. Ruhusa hii inaitwa Kighairi cha Idhini ya Ufahamu, au EFIC. Pindi tu mtu aliyeandikishwa anapopata nafuu na anaweza kutoa idhini au familia yake inawasili hospitalini, watafiti wataomba idhini ya kuendelea na utafiti. Kwa taarifa zaidi kuhusu EFIC, tafadhali tembelea: <https://www.litesnetwork.org/projects/emergency-research>

Je, ninaweza kujiondoa kwenye utafiti vipi?

Unaweza kujiondoa kwenye utafiti kwa kupiga simu 1-800-664-0557, kutuma barua pepe PAINstudy@edc.pitt.edu, au kwa kujaza fomuli iliyo chini ya www.LITESnetwork.org/PAIN ili Mtandao wa LITES ukupe bangili ya hypoallergenic silicone uvae inayoashiria kwamba hupaswi kuandikishwa katika utafiti.

Ikiwa ungependa kukataa ushiriki katika utafiti kutokana na jeraha, unaweza kukataa wakati wa tiba na EMS. Tafadhali fahamu kwamba kujiondoa kwenye utafiti kunamaanisha tu kwamba hutakuwa sehemu ya utafiti. Kujiondoa hakutakuzuia kupata dawa ya maumivu kama sehemu ya utunzaji wako wa kawaida.

Je, ni nini kinachotokea ikiwa mtu anapata bangili ya kujiondoa, lakini haivai wakati wa kuchukuliwa na EMS?

Ukipokea bangili ya kujiondoa lakini huivai wakati wa jeraha lako, inawezekana ukaandikishwa katika utafiti, isipokuwa wewe au mtu mwingine anayeandamana nawe aseme kwamba hutaki kushirikishwa katika utafiti. Hii ikitokea, huenda ukapata dawa ya utafiti, fentanyl citrate au ketamine hydrochloride, ambayo kwa kawaida hupewa wagonjwa waliojeruhiwa kutibu maumivu.

Tafadhali fahamu kwamba kujiondoa kwenye utafiti kunamaanisha tu kwamba hutakuwa sehemu ya utafiti huu. Kujiondoa hakutakuzuia kupata dawa ya maumivu (ikiwa ni pamoja na moja ya dawa hizi mbili) kama sehemu ya utunzaji wako wa kawaida.

Nikiamua kushiriki katika simu za kufuatilia, je, majukumu yangu wakati wa kipindi cha ufuatiliaji cha miezi 6 ni gani? Je, vipimo na miadi ninayopaswa kutarajia ni gani?

Ufuatiliaji wa miezi sita ni wa hiari kabisa. Ikiwa hutaki kushiriki, timu ya utafiti haitawasiliana nawe.

Ikiwa ungependa kushiriki na kutoa idhini, hakuna vipimo wala miadi ya matibabu ya ziada. Badala yake, utaipa timu ya utafiti taarifa za mawasiliano na ujaze utafiti kuhusu maumivu, wasiwasi na dawa za maumivu uliyopitia. Timu ya utafiti itawasiliana nawe tena baada ya miezi 3 na 6 ili kuuliza maswali yaleyale kuhusu maumivu ya sasa, dawa za maumivu, wasiwasi na maradhi ya msongo wa mawazo baada ya kiwewe. Unaweza kuchagua kuacha kushiriki katika tafiti hizi wakati wowote.

Je, ni nini kitakachotokea mtu akichagua kutoshiriki?

Ushiriki katika utafiti unaweza kusimama wakati wowote – mgonjwa au mwanafamilia anayefaa anahitaji tu kuiambia timu ya utafiti.

Ikiwa mgonjwa, au mwanafamilia wake hana uwezo, anasema kwamba hataki kushiriki, hiyo ni haki yake. Hii ikitendeka kabla ya kupewa dawa ya utafiti, mgonjwa atatibiwa kulingana na utunzaji wa matibabu wa wastani kwa hali yake ikiwa ni pamoja na kupokea dawa ya maumivu inayoweza kujumuisha fentanyl citrate au ketamine hydrochloride.

Katika hospitali, mfanyakazi wa utafiti atamwelezea mgonjwa na wanafamilia wake kuhusu utafiti na kuomba idhini ili mgonjwa aendelee kuwa katika utafiti. Ikiwa mgonjwa, au mwanafamilia wake atakosa uwezo, hatatoa idhini wala kubainisha kwamba hataki kushiriki wakati wa mazungumzo haya au wakati wowote baada ya kupewa dawa ya utafiti, ukaguzi wa rekodi zake za matibabu (kwa ajili ya usalama na kuona ikiwa dawa moja inaweza kuwa bora kuliko nyingine) utasimama na hatakamilisha utafiti.

Ikiwa nimeandikishwa katika utafiti, nitaweza kufahamu dawa niliyopokea?

Wagonjwa waliojiandikisha katika tafiti za EFIC zilizoidhinishwa na FDA kwa jumla hawaambiwi dawa walizopokea wakati utafiti ni wa siri. Hii inamaanisha hakuna mgonjwa wala daktari wake anaambiwa dawa inayotolewa kuzuia upendeleo wowote dhidi ya dawa. Mgonjwa na daktari watafahamishwa kwamba mgonjwa alipata dawa ya utafiti, ambayo ni fentanyl citrate au ketamine hydrochloride. Dawa zote mbili zinatumiwa sana kutibu maumivu. Kitu kikitokea ambapo daktari anayemtunza mgonjwa anahitaji kujua dawa aliyopewa, kuna mpango wa kutoa taarifa hizo haraka.

Je, inawezekana kwamba utafiti wa siku zijazo unaweza kuwapa wagonjwa chanjo bila idhini?

Utafiti wa PAIN si jaribio la chanjo na utafiti wa chanjo hautumiki kwa Mtandao wa LITES. Kwa hivyo, hatuwezi kubahatisha kuhusu chanjo kutathminiwa na utafiti wa Kighairi cha Idhini ya Ufahamu.